# STANDARD 7 KISWAHILI
# MID-TERM 1 2020

## MAAGIZO KWA WATAHINIWA
## SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI .

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu, andika katika kijitabu hiki.
3. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU.**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:

**JINA LAKO**

**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani nambari ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu, na usiikunje.
9. Kwa kila swali **1-50**, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

19. Milima mingi ikiwa pamoja huitwa ____________.

A. safu

B. korija

C. numbi

D. milima

Jibu sahihi ni **C**

Katika karatasi ya majibu

16. [A] [B] [C] [D]   17. [A] [B] [C] [D]   18. [A] [B] [C] [D]   19. [A] [B] [C] [D]

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kujazia nafasi zilizowachwa wazi.***

Jioni __1__ baada ya kula __2__, nilishika tariki kuelekea kwa Mzee Ojwang. Familia hii ilikuwa __3__ kifo cha mzee huyu. Niliwapa __4__ kisha nikaonyeshwa mahali __5__ pa kuketi. Mzee Ojwang aliaga dunia akiwa na umri wa miaka tisini na __6__. Familia hii ilijitolea sana baada ya kuona vile majirani walivyowasabilia. Kweli __7__.

1. **A.** huo **B.** hiyo **C.** hilo **D.** hicho
2. **A.** staftahi **B.** kisebeha **C.** kiamshakinywa **D.** chajio
3. **A.** inaomboleza **B.** itaomboleza **C.** ikiomboleza **D.** unaomboleza
4. **A.** mkono wa tanzia **B.** mkono wa tahania **C.** mkono wa heri **D.** mkono mwepesi
5. **A.** msafi **B.** pasafi **C.** kusafi **D.** safi
6. **A.** nane **B.** minane **C.** tatu **D.** mbili
7. **A.** vyote ving'aavyo si dhahabu **B.** aliye kando haangukiwi na mti **C.** heri jirani kuliko ndugu wa mbali **D.** ukibebwa usilevyelevye miguu

Mfumo __8__ wa elimu __9__ kuinua vipawa __10__ wanafunzi. __11__ wanafunzi wanaelewa masuala ya darasani pekee __12__ kujua utekelezaji wake. Kwa sasa mwanafunzi anahitaji kujua mambo __13__. Kuna wale watakuwa __14__ wa kutengeneza fanicha kama vile __15__.

8. **A.** mipya **B.** jipya **C.** mpya **D.** kipya
9. **A.** imenuiwa **B.** umenuiwa **C.** limenuiwa **D.** zimenuiwa
10. **A.** vya **B.** za **C.** la **D.** cha
11. **A.** Baada ya **B.** Baadhi ya **C.** Miongoni wa **D.** Kati ya
12. **A.** na **B.** kwa **C.** za **D.** bila
13. **A.** mingi **B.** vingi **C.** mengi **D.** nyingi
14. **A.** wahandisi **B.** maseremala **C.** manahodha **D.** makuli
15. **A.** kaptura na magauni **B.** sufuria na vikombe **C.** mikufu na bangili **D.** madawati na madirisha



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi***

**16.** **Andika kwa ukubwa:**

Ng'ombe wa kijijini wameumiza mtoto.

A. Ng'ombe za vijijini ameumiza mtoto.

B. Gombe la jijini limeliumiza toto.

C. Magombe ya jijini yaliliumiza toto.

D. Magombe ya jijini yaliliumiza kitoto.

**17.** Ni sentensi ipi iliyo na **'o'** rejeshi tamati?

A. Mwanafunzi aliyekuja ni mwerevu.

B. Walao kwa vijiko hawachomeki mikono.

C. Vitabu vilivyonunuliwa vimetiwa majalada.

D. Wafanyakazi waliostaafu walipewa kiinua mgongo.

**18.** **Chagua orodha iliyo na viungo vya mapishi pekee:**

A. Sahani, vijiko, mwiko, sufuria.

B. Sukari, chumvi, maji, mafuta.

C. Nyama, karoti, unga, supu.

D. Vitunguu, nyanya, mdalasini, pilipili.

**19.** **Tambua matumizi ya karibu:**

Alikula karibu machungwa kumi akiwa peke yake.

A. Karibu ya idadi.

B. Karibu ya nusura.

C. Karibu ya muda hauko mbali.

D. Karibu ya makaribisho.

**20.** **Andika wingi wa sentensi ifuatayo:**

Fundi wa mjini aliunda meza akauza.

A. Fundi wa mjini waliunda meza wakauza.

B. Mafundi wa mijini waliunda meza wakauza

C. Fundi wa mijini waliunda mameza wakauza

D. Mafundi wa mijini waliunda meza wakauza.

**21.** Bangili huvaliwa

A. shingoni

B. mkononi

C. puani

D. sikioni

**22.** Nahau <u>kula mwata</u> ina maana gani?

A. Kukosa ulichotarajia.

B. Kupata taabu.

C. Kupokea hongo.

D. Kuishiwa na pesa.

**23.** Chagua kundi lenye <u>vivumishi</u> pekee.

A. Zetu, mzuri, bora, vyenyewe, watatu.

B. Bali, bighairi ya, sembuse, ijapokuwa.

C. Taratibu, upesi, sokoni, kumi.

D. Hewala, karibu, kunradhi, makiwa.

**24.** **Bainisha aina ya maneno yaliyopigiwa kistari katika sentensi hii:**

Mtoto wake <u>alilia sana</u>.

A. Kitenzi, kielezi.

B. Kivumishi, kielezi.

C. Kielezi, kivumishi.

D. Kiunganishi, kielezi

**25.** **Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa**

"Kesho tutaenda kwetu tumwone mzazi wako," alimwambia

A. Alimwambia kuwa kesho tutaenda kwao tumwone mzazi wake.

B. Alimwambia kuwa kesho wangeenda kwao kumwona mzazi wake.

C. Alimwambia kwamba siku iliyofuata wangeenda kwao wamwone mzazi wake.

D. Walimwambia kuwa siku itakayofuata wangeenda kwao kumwona mzazi wake.



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

26. Kabati, kufuli na gari ni majina yaliyo katika ngeli ya
A. LI-YA
B. YA - YA
C. I - ZI
D. U - YA

27. Jina **mdhamini** lina silabi ngapi?
A. 5
B. 7
C. 4
D. 8

28. Ni maneno yapi ambayo <u>yote</u> ni viunganishi?
A. Ingawa, tano, meza, isipokuwa.
B. Huyu, hao, zile, pale.
C. Ila, ingawa, lakini, maadamu.
D. Sana, upesi, haraka, taratibu.

29. Salamu 'shikamoo' hujibiwa 'marahaba' ilhali 'alamsiki' hujibiwa.
A. Nawe pia
B. Jaala
C. Inshalla
D. Binuru

30. Dada yake mama huitwaje?
A. Shangazi
B. Halati
C. Mpwa
D. Mkoi

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Nchi takribani zote barani Afrika zilionja utanda wa kikoloni. Katika utawala huo watawaliwa walitiwa woga na kuaminishwa kuwa wao ni duni. Wakafikirishwa kuwa ngozi yao nyeusi ilikuwa si chochote cha maana ila imeshamiri umaskini. Wazungu nao wakajiona werevu kuliko Waafrika. Wakajifanya wavumbuzi bora. Ati ndio walivumbua mlima Kenya na Kilimanjaro. Wao hata wakasahau kuwa kulikuwa na Waafrika waliokuwa wakiishi katika bara hili na karibu na hiyo milima tangu kuzaliwa kwao.

Kusema ukweli, miaka mingi imepita na juhudi nyingi zimefanywa kuliimarisha bara hili na mafanikio yamedhihirika hapa na pale lakini ipo haja ya kujizatiti zaidi na kujiamini. Ni jambo la kuvunja moyo kuona bado hatujiamini. Kasumba za kikoloni zipo. Mwafrika akivumbua chochote lazima kwanza kiidhinishwe na mzungu. Vifaa bora vikitengenezewa Afrika lazima vitafutiwe namba za kigeni ili zivutie wanunuzi. <u>Ajabu ni kuwa wanunuzi ni hao hao Waafrika</u>. Tunapaswa kutambua kuwa hata sisi tunao uwezo wa kuyaboresha mabara mengine. Turingie bidhaa na uwezo wetu.

Tuepuke sana utegemezi. Na ni utegemezi wa aina zote. Ule wa kiuchumi, kiakili, kisiasa na hata kielimu. Wakati umefika wa vitendo vya kujiendeleza. Tupendane na wazungu kama marafiki walio sawa lakini sio kati ya rafiki mnyonge na mwenye nguvu. Tukiuondoa udhaifu huu tutakuwa sambamba na watu hao. Ni vyema hata wao watambue kuwa sote ni binadamu kama wao. Bila shaka wengi wa hao weupe siku hizi wanajua kuwa tunao uwezo na tunazidi kupendana nao.

Ukweli ni kwamba, viongozi wengi wa Kiafrika wamepevuka na wanaujua umuhimu wa kuringia utamaduni wetu. Wanapaswa wautumie uwezo wao wote kuzirekebisha hali. Wanafahamu bara letu la Afrika lina <u>malighafi</u>



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

gani. Hivyo basi yapasa nchi za kiafrika zibadilishane malighafi. Watu watumie vipawa vyao vizuri, waimarishe ufundi na elimu nyinginezo kujiboresha kiuchumi badala ya kuwakimbilia hao wakoloni wakongwe huko ulaya. Fikira za kikasuku za kuwa waafrika hawawezi chochote zifukiwe katika kaburi la liliwala. Hazina mashiko yoyote.

Wacha niseme hapa kuwa, huu si wakati wa kupambana kidhaifu bali ni wakati wa Afrika kujikuza na kujiingiza katika mstari wa mbele wa nchi zilizoendelea lakini si miongoni mwa zile maskini. Ifahamike kuwa, tukizorota hivi, mataifa katika mabara yale mengine yatakuwa yanapiga kasi za umeme kiuchumi.

Bara la Afrika limebarikiwa na watu wenye vipawa anuwai, mali ya asili yenye thamani kubwa, mathalani mafuta, gesi, dhahabu, almasi, shaba na madini mengi. Aidha tuko na maeneo mengi ya kuendelezea utalii. Sehemu za kuendeleza kilimo ni nyingi. Hatuna theluji ambazo huwazuia watu kulima.

Ili ufanisi huu uweze kufikia upeo mkubwa, lazima sekta ya mawasiliano iimarishwe. Miundo msingi yote idhibitiwe vyema. La muhimu kila Mwafrika ajivunie Uafrika wake.

---

**31.** Aya ya kwanza inatudokezea kuwa,

A. nchi zote barani Afrika zilitawaliwa na wakoloni.

B. karibu nchi zote za bara la Afrika zilitawaliwa na wakoloni.

C. hakuna nchi yoyote barani Afrika ambyo ilitawaliwa na wakoloni.

D. ni nchi chache sana katika bara la Afrika zilitawaliwa na wakoloni.

**32.** Kulingana na kifungu hiki,

A. wazungu ndio waliovumbua mlima Kenya lakini si mlima Kilimanjaro.

B. wazungu ndio walivumbua mlima Kilimanjaro lakini si mlima Kenya.

C. wazungu hawakuvumbua mlima wowote.

D. wakoloni hawakulitawala taifa lolote katika bara la Afrika.

**33.** Ajabu ni kuwa wanunuzi ni hao hao Waafrika. Hii ni mbinu gani ya uandishi?

A. Kinaya

B. Chuku

C. Majazi

D. Istiara

**34.** Ni wazi kuwa,

A. waafrika wote wanajiamini.

B. waafrika bado hawajiamini.

C. wakoloni bado wanatupenda.

D. wakoloni wengi bado hawajiamini.

**35.** Waafrika wanahimizwa kuepuka mtegemezi ufuatao ila

A. wa kiuchumi

B. wa kisiasa

C. wa kielimu

D. wa ubinafsi



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**36.** Viongozi wengi wa Kiafrika,

A. wamepevuka na wanajua umuhimu wa kuringia utamaduni wetu.

B. ni wabinafsi na ndio wanyanyasaji wakuu baada ya wakoloni kuondoka.

C. hawajajua thamani ya Mwafrika wala thamani ya utamaduni wake.

D. ni wachoyo na hawana malengo yoyote bora ya kuliimarisha bara letu la Afrika.

**37.** Malighafi hutumiwa

A. nyumbani

B. shuleni

C. hospitalini

D. viwandani

**38.** Kifungu hiki kinadhamiria kutuonyesha kuwa

A. mwafrika ni mjinga asiyejua chochote wala lolote.

B. mwafrika ana akili kama mzungu na anaweza hata kufanya makubwa kuliko mzungu mwenyewe.

C. mzungu amebarikiwa na akili tambuzi tofauti ni sisi waafrika.

D. mwafrika hana thamani yoyote na daima humtegemea mzungu.

**39.** Kilimo barani Afrika

A. kinaweza kufanyika vizuri kwa kuwa hakuna theluji.

B. kinaathiriwa sana na hali ya anga na baridi kali.

C. kiko na changamoto nyingi sana za hapa na pale.

D. hufanyika wakati wa mafuriko pekee.

**40.** La muhimu kila Mwafrika ajivunie Uafrika wake. Ni methali gani inayoafiki kauli hii?

A. Mjumbe hauwawi.

B. Mtegemea cha nduguye hufa maskini.

C. Asiye na wake ana Mola.

D. Mwacha mila ni mtumwa.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Petero alikuwa nyumbani akiwaza na kuwazua kuhusu hali ya baba yake. Alianua kwenda kumshughulikia baba yake ambaye alikuwa habanduki kitandani kutokana na maradhi na pia uzee. Usisahau kuwa ni juzi tu baba yake alikuwa akijifanyia kazi zake zote kutoka kulisha mifugo machungani na kuendesha trekta lake la kulimia. Ilikuwa nadra sana baba yake kuhitaji usaidizi wowote. Petero alikumbuka vile baba yake alivyokuwa na nguvu katika enzi zake za awali. Siku hii husika nayo alikuwa hoi hata kumwinga nzi aliyetua usoni na kero zake hangeweza. Baba yake alikuwa akiwategemea wengine kwa shughuli zake hizi. Hapa ya wahenga yakadhihirika kuwa ujana ni moshi ukienda haurudi.

Petero alipokuwa akiwaza haya, alisikia mbisho mlangoni. Alikimbia kumlaki. Aha! Kumbe alikuwa ni mjomba wake. Licha ya umri wake, mjombawe alikuwa amewahi mapema kama ilivyokuwa kawaida yake kumjulia hali shemeji yake. Baada ya kujuliana hali, mjomba alianza mazungumzo marefu ambayo Petero hakujua iwapo



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

yalikuwa pongezi au mawaidha.

"Mtoto wetu, nyinyi ni vijana wa kipekee sana. Ni muhali kupata vijana kama nyinyi hasa katika janibu hizi. Licha ya kazi zenu, wewe na ndugu zako hamchoki kuja kuwasaidia wazazi wenu na kuwakimu. Dadangu huniambia kuwa hakuna kitu wanachokikosa. Hata sasa baba yenu yu katika hali mahututi hamkomi kuja kumletea dawa na kumjulia hali. Nyinyi watoto wa dadangu mmepigiwa mfano katika kijiji kizima. Kuona vile mnajitolea kuwatunza wazazi wenu vikongwe ni jambo linalotia fora. Wazazi wengi kijijini wanawaomba watoto wao wawe kama nyinyi. Langu ni kumhimiza msikate tamaa.

Hebu angalia katika kijiji chetu. Tuna watu wengi waliosoma na wanafanya kazi za hadhi kote nchini. Lakini wametelekeza wazazi wao. Wewe umeshuhudia binamu zako baada ya kwenda ughaibuni jinsi walivyowatelekeza wazazi wao. Usisahau wazazi hao hao ndio waliowaelimisha. Walipoelimika, wakawatoroka wazazi na kwenda nchi za mbali ambazo wazazi hawawezi kufika. Hebu fikiria hata hawakuweza kufika katika mazishi ya wazazi wao. Ni wengi sana ambao wamehuzunishwa na jambo hilo. Hivi mnavyowalinda wazazi wenu ni jambo la kutia moyo. Pengine ni kweli wahenga walivyosema kuwa kwa kawaida mtoto huiga tabia za wazazi wake. Ona hata dada yetu hakuwatelekeza wazazi wake. Wengine wetu tukihangaika na dunia, yeye alikuwapo kuwahudumia hadi dakika za mwisho. Namwombea wapwa wangu muendelee na moyo uo huo."

**41.** Ni jambo gani lililomfikirisha Petero kufika pale nyumbani?
A. Mgeni aliyeingia ndani ya nyumba yao bila kutarajiwa.
B. Hali ya afya ya baba yake mzazi.
C. Hali ngumu ya maisha kwa kukosa mahitaji muhimu ya kimsingi.
D. Ndugu zake ambao walikuwa wametelekeza mzazi wao.

**42.** Aya ya kwanza inatuonyesha kuwa,
A. kifo huwa karibu sana wakati wowote.
B. marafiki wanaweza kumtoroka lakini ndugu hawezi.
C. watoto huwa na huruma kuliko watu wakubwa.
D. nguvu za mwili huisha jinsi uzee unavyoingia.

**43.** Ni wazi kuwa baba yake Petero alipokuwa kijana
A. alienziwa sana na wakazi wa eneo hilo.
B. alipenda kuwasumbua wenzake sana kutokana na nguvu zake.
C. hakuhitaji usaidizi wowote kwa kuwa tayari alikuwa na nguvu zake.
D. alikuwa mnyanyasaji kupindukia asiyejali mali ya wengine.

**44.** Ni 'muhali' ina maana ya
A. ni vigumu
B. ni rahisi
C. ni vizuri
D. ni vibaya



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**45.** Petero na ndugu zake,

A. waliwatelekeza wazazi wao.

B. waliwatekelezea wazazi wao yaliyohitajika.

C. hawakuwashughulikia wazazi wao masuala muhimu.

D. waliwapendeza majirani kuliko wazazi wao.

**46.** Kwa nini Petero na nduguze wanapigiwa mfano katika kijiji kizima?

A. Hawashughulikii wazazi wao.

B. Waliwashughulikia sana wazazi wao.

C. Walikuwa watovu wa nidhamu.

D. Walikuwa wakiburura mkia darasani.

**47.** Ni nini maana ya <u>msikate tamaa</u>?

A. Msifurahie dhiki za wengine.

B. Msiwasahau wazazi wenu.

C. Msipoteze matumaini.

D. Msilegeze juhudi.

**48.** Kulingana na aya ya mwisho,

A. mzazi akimsomesha mtoto wake vizuri, huwa amejiwekea akiba.

B. ni vigumu mzazi amsomeshe mtoto wake vizuri kisha mtoto akose kumsaidia.

C. wazazi wasiowasomesha watoto wao ndio huteseka sana katika maisha.

D. Si lazima mtoto amsaidie mzazi wake ati kwa kuwa mzazi amemsomesha.

**49.** Wapwa ni

A. watoto wa ndugu.

B. watoto wa shangazi.

C. watoto wa mjomba.

D. watoto wa halati.

**50.** <u>Kwa kawaida mtoto huiga tabia za wazazi wake</u>. Ni methali gani inayolenga kauli hii?

A. Mtoto wa yungi hulewa sembuse wa binadamu.

B. Kila chambo na wimbile.

C. Mwana hutazama kisogo cha ninaye.

D. Msafiri ni aliye pwani.



**Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | Tel:+254202319748**
E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com